



WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

TAARIFA KWA UMMA

UHAKIKI WA TAARIFA ZA WAMILIKI WA ARDHI NCHINI

Wizara ya Ardhi Nyumba na Maendeleo ya Makazi inatoa taarifa kwa Umma kwamba inaendelea na zoezi la uhakiki wa taarifa za wamiliki wa ardhi nchini lililoanza tarehe **01 Julai, 2021**. Wamiliki wa ardhi wanaohusika katika zoezi hili ni wamiliki wenye:-

1.	Hatimiliki,
2.	Barua za Toleo za muda mrefu au mfupi; na
3.	Leseni za Makazi.

Zoezi la uhakiki wa taarifa za wamiliki wa ardhi litaratibiwa kwenye Ofisi za Ardhi za Mikoa na Halmashauri za Majiji, Manispaa, Miji na Wilaya kote nchini. Wamiliki wote wa ardhi wanatakiwa kujaza taarifa zao za umiliki wa ardhi kwenye dodoso maalum linalopatikana katika ofisi tajwa au kwenye tovuti ya Wizara (www.lands.go.tz). Dodoso lenye taarifa na viambatisho vyake liwasilishwe kupitia ofisi hizo au barua pepe ya occupancy@lands.go.tz. Ili kufanikisha zoezi hili, wamiliki wa ardhi wanatakiwa kuwasilisha nyaraka zifuatazo wakati wa uhakiki:

1.	Vivuli vya Hatimiliki au Barua ya Toleo au Leseni ya Makazi;
2.	Kivuli cha Kitambulisho cha Taifa (NIDA) au namba ya NIDA;
3.	Iwapo mmiliki ni Kampuni au Taasisi; Vivuli vya Hati ya Usajili, taarifa za wanahisa na Vitambulisho vya Taifa vya wanahisa.

Wamiliki wa ardhi ambao watahondwa kuwasilisha taarifa zao wenyewe kutokana na sababu mbalimbali, wanaruhusiwa kuwasilisha taarifa kupitia kwa wawakilishi wao ambao watawatambulisha kwa barua rasmi. Zoezi hili limepangwa kufanyika kwa muda wa miezi mitatu (3) kuanzia tarehe **1 Julai, 2021** mpaka **30 Septemba, 2021**.

Imetolewa na'-

Mary G. Makondo
KATIBU MKUU



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA
NA MAENDELEO YA MAKAZI

DODOSO LA KUHAKIKI WA TAARIFA ZA WAMILIKI ARDHI

(Ijazwe na Wamiliki wa Ardhi)

- 1.0. Jina la mmiliki/Wamiliki na Anwani.....
- 1.1. Namba ya simu.....Barua Pepe..... Mtaa/Kijiji unapoishi.....
- 1.2 Taja namba ya kiwanja/Shamba unalolimilikiKitalu.....Mahali.....Halmashauri.....
Mkoa.....Hati Na..... Tarehe ya mwisho ya kulipia kodi ya pango la ardhi.....
- 1.3. Je unamiliki kama Kampuni, Taasisi Zisizo za Kiserikali (NGO's), Taasisi za Kijamil (CBO's), Taasisi zilizo chini ya Bodi za wadhamini?
a) Ndiyo ()
b) Hapana ()
Kama ni ndiyo taja majina ya wanahisa/ wadhamini pamoja na uraia wao;
i. Uraia.....
ii. Uraia.....
iii. Uraia.....
iv. Uraia.....
- 1.4. Taja Majina ya mmiliki/wamiliki yaliyopo kwenye Kitambulisho cha Taifa kutoka NIDA na namba yake;
i. Majina.....Namba ya NIDA.....
ii. Majina.....Namba ya NIDA.....
iii. Majina.....Namba ya NIDA.....
iv. Majina.....Namba ya NIDA.....
- 1.5 Kama majina ya kitambulisho cha NIDA ni tofauti na yaliyopo kwenye Hati/Leseni ya Makazi/ Barua ya Toleo (Offer) ambazo unamiliki/mnamiliki, toa sababu kwa kuweka alama ya (v) (unaweza kuweka kwa zaidi sababu moja):
a) Kutohamisha miliki (transfer); ()
b) Kukosewa/kutohuishwa kwa majina kwenye Mifumo ya Wizara ()
c) Mmiliki kutofikisha umri wa miaka 18 ()
d) Kurithi ()
e) Sababu nyingine (eleza tafadhali).....
- 1.6 Je, unamiliki/mnamiliki viwanja/mashamba kwenye maeneo mengine hapa nchini? (Jaza kwenye jedwali na ambatanisha na nakala ya Hatimiliki/Leseni/Barua ya Toleo (Offer) husika). Iwapo nafasi haitoshi geuza nyuma ya karatasi hii.

Na;	1.6.1 Namba ya Kiwanja/Shamba	1.6.2 Kitalu	1.6.3 Mahali/Eneo	1.6.4 Hati Na	1.6.5 Jina/Majina	1.6.6 Halmashauri	1.6.7 Mkoa	1.6.8 Tarehe ya Mwisho kulipia kodi ya pango la ardhi
1.								
2.								
3.								
4.								
5.								

1.1.7 VIAMBATISHO

Tafadhali pamoja na maelezo uliyoyajaza hapo juu ambatisha vivuli/nakala ya nyaraka zifuatazo:

- a) Barua ya Toleo(Offer), Leseni ya Makazi au Hatimiliki ya eneo unalomiliki;
b) Kitambulisho cha NIDA;
c) Cheti cha Usajili na Nyaraka zinginezo kwa Makampuni, NGO,CBO,Taasisi;
d) Uraia wa Wanahisa au Wadhamini kwa Makampuni, NGO,CBO,Taasisi.